TAMKO LA MKUU WA MKOA WA KILIMANJARO KUZUIA USAFIRISHAJI WA MPUNGA, MCHELE, MAHINDI, UNGA WA MAHINDI NA SUKARI KWENDA NJE YA NCHI

UONGOZI WA MKOA WA KILIMANJARO UNAPENDA KUWATANGAZIA WANANCHI WOTE WA MKOA WA KILIMANJARO HUSUSANI WAFANYABIASHARA WA SUKARI NA MAZAO YA NAFAKA ZA MPUNGA, MAHINDI, MCHELE NA UNGA WA MAHINDI KUWA, **NI MARUFUKU KWA MFANYABIASHARA YEYOTE AU MWANANCHI YEYOTE KUSAFIRISHA BIDHAA ZILIZOTAJWA KWENDA NJE YA NCHI BILA KIBALI CHA SERIKALI.**

KUWA, KUFANYA HIVYO NI KUHUJUMU UCHUMI WA NCHI KAMA ILIVYOAINISHWA KWENYE **KIFUNGU CHA TATU (3)** CHA JEDWALI LA KWANZA LA SHERIA YA UHUJUMU UCHUMI **SURA YA 200** YA SHERIA ZA TANZANIA. AIDHA HII NI KUKIUKA AGIZO LA MHESHIMIWA WAZIRI MKUU KUPITIA WARAKA WAKE WA TAREHE **30 MEI, 2017 WA KUZUIA UTOKAJI WA VYAKULA NA SUKARI KWENDA NCHI JIRANI** NA PIA MAELEKEZO YAKE ALIYOYATOA TAREHE 26/06/2017 WAKATI WA BARAZA LA EID-EL-FITRI LILILOFANYIKA MJINI MOSHI NA KUWA, KUFANYA HIVYO KUNAWEZA KUSABABISHA UPUNGUFU WA CHAKULA KWENYE BAADHI YA MAENEO HAPA NCHINI NA KUSABABISHA MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (TRA) KUKOSA TAKWIMU MUHIMU ZA BIDHAA ZINAZOSAFIRISHWA NJE.

OFISI YANGU IMEJIRIDHISHA KUWA, BAADHI YA WAFANYABIASHARA WAMEKUWA WAKISAFIRISHA SUKARI/NAFAKA HIZO NYAKATI ZA USIKU KUPITIA NJIA AMBAZO SI RASMI KWA KUSHIRIKIANA NA BAADHI YA ASKARI POLISI AMBAO SIO WAAMINIFU. AIDHA, BAADHI YA WAFANYABIASHARA HUTOA MAELEZO KUWA, WANAYO MAGHALA YA CHAKULA KATIKA MAENEO YA MIPAKA YETU NA NCHI YA KENYA. HIVI KARIBUNI, SHEHENA YA MAHINDI IMEKAMATWA WILAYA YA SIHA IKIWA INASAFIRISHWA USIKU WA MANANE KWA MAELEZO KUWA ILIKUWA INAPELEKWA KWENYE MAGHALA YALIYOKO TARAKEA.

JAMBO LA KUSTAJAABISHA NI KUWA, SHEHENA HIYO ILIKUWA INASAFIRISHWA USIKU KWENDA TARAKEA KUPITIA NJIA YA SIHA – NGARENAIROBI – KAMWANGA – TARAKEA AMBAYO NI YA VUMBI YENYE

UMBALI MREFU IKILINGANISHWA NA BARABARA YA MOSHI – ROMBO – TARAKEA YENYE UMBALI MFUPI AMBAYO NI YA LAMI .

AIDHA, TAARIFA ZA OFISI YANGU ZINAONYESHA WILAYA YA ROMBO HAINA UHABA WA CHAKULA, NA HIVYO HII INAONYESHA WAZI KUWA NI MTANDAO WA BIASHARA YA MAGENDO YA MAZAO YA CHAKULA KWENDA NCHI JIRANI.

VILE VILE OFISI YANGU INAPENDA KUTOA TAARIFA KUWA, HALI YA MAVUNO YA MAZAO YA CHAKULA YA MSIMU WA **2015/2016,** AMBACHO NDICHO CHAKULA KINACHOENDELEA KUTUMIKA HADI SASA, MKOA WA KILIMANJARO HAUNA UHABA WA CHAKULA, BALI UNA ZIADA YA TANI **62,468** ZA WANGA NA TANI **4,522** ZA PROTINI. WILAYA YA ROMBO ILIYOKO MPAKANI INA ZIADA YA CHAKULA TANI **14,648** ZA WANGA NA TANI **8,000** ZA PROTINI. JAMBO AMBALO HALISHAWISHI MFANYABIASHARA WA MAHINDI KUFANYA BIASHARA KATIKA ENEO HILO.

KWA UPANDE MWINGINE BEI ZA MAHINDI ZINAONYESHA KUWA WILAYA YA ROMBO, GUNIA LA MAHINDI LINAUZWA KATI YA SHILINGI **75,000 - 80,000** IKILINGANISHWA NA WILAYA YA MOSHI NA SIHA AMBAKO GUNIA LA MAHINDI LINAUZWA KATI YA SHILINGI **105,000 - 120,000**. HIVYO NI MATARAJIO YETU KUWA WAFANYABIASHARA HALALI WANATARAJIWA KUSAFIRISHA MAHINDI KWENDA SIHA NA MOSHI KULIKO ROMBO AMBAKO BEI YA MAHINDI IKO CHINI. HATA HIVYO BADO YAPO MAENEO NDANI YA NCHI YENYE UHITAJI MKUBWA WA MAZAO YA NAFAKA.

OFISI YANGU INAZO TAARIFA KUWA WAPO WANANCHI WANAOUZA MAZAO YAKIWA MASHAMBANI. NIWAOMBE WANANCHI KUEPUKA KUUZA MAZAO YAKIWA SHAMBANI NA KUEPUKA WAFANYABIASHARA WANAONUNUA MAZAO KWA BEI ZA CHINI KWA KIPINDI HIKI CHA MAVUNO. NAWATAKA MUWE NA SUBIRA NA KUUZA MAZAO HAYO KWA BEI NZURI KWA VIPIMO VILIVYOTHIBITISHWA.

KUFUATIA HALI HIYO, NINAAGIZA KUWA:-

(i) NI MARUFUKU KUSAFIRISHA SUKARI, MAHINDI, MCHELE, MPUNGA NA UNGA WA MAHINDI NDANI YA MKOA WAKATI WA USIKU;

(ii) MWANANCHI YEYOTE AU MFANYABIASHARA YEYOTE ATAKAYEKAMATWA AKISAFIRISHA SUKARI, MAHINDI, MPUNGA, MCHELE NA UNGA WA MAHINDI KWENDA NJE YA NCHI ATACHUKULIWA HATUA KALI KULINGANA NA SHERIA YA UHUJUMU UCHUMI SURA YA 200 YA SHERIA ZA TANZANIA. AIDHA, MAZAO HAYO YATATAIFISHWA NA KUPELEKWA KWENYE GHALA LA CHAKULA LA TAIFA KULINGANA NA AGIZO LILILOTOLEWA NA MHE. WAZIRI MKUU TAREHE 26/06/2017;

(iii) WAFANYABIASHARA WOTE WAACHE BIASHARA YA KUSAFIRISHA MAZAO NJE YA NCHI BALI WAZITUMIE FURSA ZILIZOPO KATIKA SOKO LA NDANI KUKIDHI MAHITAJI YAO YA KIBIASHARA;

(iv) MAGARI YOTE YATAKAYOTUMIKA KATIKA USAFIRISHAJI HUU YATAHESABIKA KUWA SEHEMU YA UHUJUMU UCHUMI. YATABAKI VITUO VYA POLISI HADI WAMILIKI WATAKAPOPATIKANA NA KUJIBU MASHTAKA DHIDI YAO;

(v) ASKARI POLISI WANAOJIHUSISHA NA SHUGHULI ZA USINDIKIZAJI PAMOJA NA KUPANGA NJIA *(ROUTE)* ZA KUSAFIRISHA MAZAO HAYO WANATAKIWA KUACHA TABIA HIYO MARA MOJA AU KUONDOKA NDANI YA JESHI LA POLISI KABLA HAWAJACHUKULIWA HATUA ZA KISHERIA;

(vi) MWANANCHI YEYOTE ANAYEJUA AU MWENYE TAARIFA KUHUSU BIASHARA HII HARAMU ANAOMBWA KUTOA USHIRIKIANO KWA VYOMBO VYETU VYA ULINZI NA USALAMA.

(vii) NI MARUFUKU KWA WAFANYABIASHARA KUNUNUA MAZAO SHAMBANI. AIDHA, IDARA YA UHAMIAJI INAPASWA KUFANYA UCHUNGUZI WA KUWABAINI WAFANYABIASHARA KUTOKA NJE WANAOJIHUSISHA NA UNUNUZI WA MAZAO MASHAMBANI.

BAADA YA AGIZO LA WAZIRI MKUU NA TAMKO HILI, WANANCHI WOTE WA MKOA WA KILIMANJARO MNAPASWA KUSHIRIKIANA KWA PAMOJA KUKOMESHA USAFIRISHAJI WA SUKARI NA MAZAO YA NAFAKA KWENDA NJE YA NCHI BILA VIBALI MPAKA PALE ITAKAPOAMULIWA VINGINEVYO.

ANNA E. MGHWIRA
MKUU WA MKOA
KILIMANJARO
28 JUNI, 2017